(NBAA)

BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU

TANZANIA

SIMU: (255) (026) 2963318-9
TELEGRAMU: (255) (022) 2151746
BARUA PEPE: info@nbaa.go.tz
TOVUTI: www.nbaa.go.tz

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI "AUDIT HOUSE", GHOROFA YA NANE, BARABARA YA UKAGUZI, S.L.P. 1271, 41104 TAMBUKARELI, DODOMA, TANZANIA

NBAA/PR.1/II/61 23.12.2019

# TAARIFA KWA UMMA
# MATOKEO YA MITIHANI YA 90 YA NBAA ILIYOFANYIKA NOVEMBA 2019

## 1.0 Utangulizi

Katika kikao cha kawaida cha 180 cha Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kilichokaa leo Jumatatu tarehe 23 Desemba 2019, chini ya Mwenyekiti wake CPA. Prof.Isaya J. Jairo, kimeidhinisha matokeo kwa watahiniwa waliofanya mitihani ya Bodi iliyofanyika tarehe kuanzia Jumanne 29 Oktoba hadi Ijumaa tarehe 01 mwezi wa Novemba 2019. Mitihani hiyo ilifanyika katika vituo kumi na moja vya mitihani vilivyopo Tanzania Bara na Visiwani. Mitihani hiyo ilihusisha watahiniwa katika hatua ya Kwanza na ya Pili katika Ngazi ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC I, ATEC II) zenye masomo manne kila moja na Ngazi ya Taaluma; Hatua ya Msingi (Foundation Level) na Hatua ya Kati (Intermediate Level) zenye masomo sita kila moja, na Hatua ya Mwisho (Final Level) yenye masomo manne. Mitihani hii ni ya kwanza baada ya kuboreshwa kwa mfumo mpya wa elimu na mafunzo unaozingatia weledi.

## 2.0 Matokeo ya mitihani

### 2.1 Matokeo ya Jumla

Watainiwa waliosajiliwa walikuwa **6,805** kati ya hao watahiniwa **626** sawa na asilimia **9.2** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **6,179** sawa na asilimia **90.8**. Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo watahiniwa **237** ambao ni asilimia **3.8** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **41** sawa na asilimia **0.7** wamefaulu kwa kufaulu masomo walioyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **921** sawa na asilimia **14.9** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **1,199** sawa na asilimia **19.4** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa wengine **2,678** sawa na asilimia **43.3** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi mbalimbali na watahiniwa **2,302** waliobakia sawa na asilimia **37.3** hawakufaulu mitihani yao.

### 2.2 Watahiniwa waliofaulu kutunukiwa Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC) na Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

#### 2.2.1 Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC)

Jumla ya watahiniwa **53** wamefaulu mtihani wa Ngazi ya Cheti (Accounting Technician Level II). Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya Cheti kufikia **3,993** tangu mitihani hii ianze mwaka 1991. Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **17** sawa na asilimia **32.1** na wanaume ni **36** sawa na asilimia **67.9.**

#### 2.2.2 Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

Jumla ya watahiniwa **325** wamefaulu mtihani wa Shahada ya Juu ya Uhasibu nchini - CPA (T). Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **138** sawa na asilimia **42.5** na wanaume ni **187** sawa na asilimia **57.5.** Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya CPA kufikia **9,666** tangu mitihani hii ianze mwaka 1975.

### 2.2.3 CPA (T) Mlingano [(CPA(T)] (Equivalent)

Jumla ya watahiniwa **17** wamefaulu mtihani wa CPA (T) Mlingano [(CPA (T)] Equivalent Qualification idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani hii kufikia **182** tangu mitihani hii ianze Novemba 2014.

## 2.3 Matokeo katika Ngazi Mbalimbali

### 2.3.1 Ngazi ya Cheti (Accounting Technician)

#### 2.3.1.1 Hatua ya Awali ya Cheti (Accounting Technician Level I)

Katika ngazi ya awali ya mitihani ya Uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC I) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **97** kati ya hao watahiniwa **12** sawa na asilimia **12.4** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **85** sawa na asilimia **87.6**.

Kati ya watahiniwa **85** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **11** ambao ni asilimia **12.9** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **17** sawa na asilimia **20.0** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **28** sawa na asilimia **32.9** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **43** sawa na asilimia **50.6** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **14** waliobakia sawa na asilimia **16.5** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.1.2 Hatua ya Pili ya Cheti (Accounting Technician Level II)

Katika ngazi ya uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC II) waliosajiliwa walikuwa **197** kati ya hao watahiniwa **24** sawa na asilimia **12.2** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani katika ngazi hii walikuwa **173** sawa na asilimia **87.8.** Kati ya watahiniwa **173** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **16** ambao ni asilimia **9.2** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **37** sawa na

asilimia **21.4** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **53** sawa na asilimia **30.6** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **67** sawa na asilimia **38.7** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **53** waliobakia sawa na asilimia **30.6** hawakufaulu mitihani yao.

### 2.3.2 Ngazi ya Taaluma (Professional Stage)

#### 2.3.2.1 Hatua ya Awali (Foundation Level)

Katika Hatua ya Awali, waliosajiliwa walikuwa **765** kati ya hao watahiniwa **77** sawa na asilimia **10.1** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **688** sawa na asilimia **89.9**. Kati ya watahiniwa **688** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa 135 ambao ni asilimia **19.6** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **04** sawa na asilimia **0.6** wamefaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **168** sawa na asilimia **24.4** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **307** sawa na asilimia **44.6** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **255** sawa na asilimia **31.7** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **126** waliobakia sawa na asilimia **18.3** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.2 Hatua ya Kati (Intermediate Level)

Katika Hatua ya Kati, waliojisaliwa walikuwa **3,685** kati ya hao watahiniwa **375** sawa na asilimia **10.2** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **3,310** sawa na asilimia **89.8**. Kati ya watahiniwa **3,310** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **33** ambao ni asilimia **1.0** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **31** sawa na asilimia **0.9** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **410** sawa na

asilimia **12.4** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **474** sawa na asilimia **14.3** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **1,529** sawa na asilimia **46.2** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **1,307** waliobakia sawa na asilimia **39.5** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.3 Hatua ya Mwisho (Final Level)

Katika Hatua ya Mwisho, waliosajiliwa walikuwa **2,061** kati ya hao watahiniwa **138** sawa na asilimia **6.7** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **1,923** sawa na asilimia **93.3**. Kati ya watahiniwa **1,923** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **42** ambao ni asilimia **2.2** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **06** sawa na asilimia **0.3** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **289** sawa na asilimia **15.0** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **337** sawa na asilimia **15.7** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **784** sawa na asilimia **40.8** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **802** waliobakia sawa na asilimia **41.7** hawakufaulu mitihani yao.

## 4.0 Watahiniwa waliobakiza muhula mmoja kutakiwa kumaliza mitihani yao katika ngazi husika

Wapo watahiniwa **232** ambao walifaulu baadhi ya masomo katika muhula wa Novemba 2017. Watahiniwa hawa wanatakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyobakia katika ngazi husika hadi Mei 2020. Hivyo wamebakiza muhula mmoja tu ili kufaulu masomo yaliyobakia la sivyo masomo waliyofaulu huko nyuma yatafutwa na kutakiwa kuanza upya ngazi husika.

## 5.0 Watahiniwa waliofutiwa masomo waliyokuwa wamefaulu

Wapo watahiniwa **140** ambao walifaulu baadhi ya masomo kuanzia muhula wa Mei 2017. Watahiniwa hawa walitakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyokuwa yamebakia katika ngazi husika kabla au katika muhula wa mitihani ya Novemba 2019. Wanafunzi hawa walishindwa kufanya hivyo na hivyo masomo waliyofaulu yamefutwa na wanatakiwa kujisajili upya kwa ajili ya mitihani hiyo. Hii inajumuisha hata wale ambao hawakufanya mitihani katika muhula huu lakini walikuwa wamefaulu baadhi ya masomo kuanzia Muhula wa Mei 2017 lakini hadi sasa hawajafaulu masomo yaliyobakia.

## 6.0 Pongezi

Bodi inawapongeza wale wote waliofuzu mitihani yao na kuwataka wale ambao hawakufaulu kutokata tamaa bali waongeze bidii zaidi katika masomo yao ili waweze kufanya vizuri katika mitihani ijayo ya Bodi. Bodi inawashauri kutumia vema vitabu vilivyotayarishwa na Bodi katika kijiandaa kwa mitihani yao. Pia wanashauriwa kusoma vitabu vingine vya ziada ili kuongeza ufahamu zaidi katika masomo hayo.

## 7.0 Mitihani inayofuata

- Mitihani ya katikati ya muhula kwa ajili ya masomo ya A5 Business Law, B5 Performance Management, C3 Corporate Finance and C4 Advanced Taxation itafanyika tarehe **Jumanne tarehe 25 na Jumatano tarehe 26 mwezi wa Februari 2020** katika kituo cha Dar es Salaam tu. Wote wanaopenda kujisajili katika mitihani hii wanakaribishwa.
- Mitihani ya kawaida itafanyika kuanzia jumanne **tarehe 5 hadi tarehe 8 Mei 2020** katika vituo vitakavyotangazwa.

## 8.0 Uwasilishaji wa picha kwa ajili ya mahafali

Mahafali ya 42 ya NBAA yatafanyika **tarehe 3 mwezi Oktoba 2020**. Tangazo rasmi kuhusu mahafali hayo litawekwa kwenye tovuti ya Bodi. Wale wote waliofaulu mitihani ya ATEC II na CPA (T) pamoja na wale wa CPA (T) Equivalent wanatakiwa kuwasilisha picha zao kwa ajili ya kutengenezewa vyeti kabla ya **tarehe 30 Januari 2020**. Tangazo juu ya namna ya kuwasilisha picha hizo liko kwenye tovuti ya Bodi.

Matokeo haya ya mitihani ya **90** ya Bodi yanapatikana katika tovuti ya NBAA ambayo ni www.nbaa.go.tz

**CPA Pius A. Maneno**
**MKURUGENZI MTENDAJI**